







*IDARA YA UPATIKANAJI WA AFYA YA VERMONT*

# Mipango ya Huduma za Afya
# Kitabu cha mwongozo

GreenMountainCare
A HEALTHIER STATE OF LIVING

## Attention! If you need help in your language, please call 1-800-250-8427

انتباه! إذا كنت بحاجة إلى مساعدة بلغتك ، فيرجى الاتصال
على **1-800-250-8427**

သတိပြုရန်! မိတ်ဆွေသည် သင့်ဘာသာစကားဖြင့် အကူအညီ လိုပါက၊
ကျေးဇူးပြုပြီး 1-800-250-8427 ကိုခေါ်ပါ။

Pažnja! Ako vam je potrebna pomoć na vašem jeziku, pozovite **1-800-250-8427**

توجه! اگر شما نیاز به کمک در زبان خود، لطفا با شماره تلفن 1-800-250-8427

Attention! Si vous avez besoin d’assistance dans votre langue, appelez le **1-800-250-8427**

Nurabe maso! Niba ukeneye ubufasha mu rurimi rwawe, wahamagara kuri **1-800-250-8427**

ध्यान! यदि तपाईंलाई आफ्नो भाषामा मद्दत चाहिन्छ भने, कृपया **1-800-250-8427** मा कल गर्नुहोस्

پاملرنه! که تاسو په خپله ژبه کې مرستې ته اړتیا لرئ،
مهرباني وکړئ **1-800-250-8427** ته زنګ ووهئ

Ogow! Haddii aad u baahan tahay in lagugu caawiyo luqaddada, fadlan wac **1-800-250-8427**

¡Atención! Si necesita ayuda en su idioma, por favor llame al **1-800-250-8427**

Tahadhali! Kama unahitaji msaada kwa lugha yako, tafadhali piga simu **1-800-250-8427**

Uvaha! Yakshcho vam potribna dopomoha vashoyu movoyu, telefonuyte za nomerom **1-800-250-8427**

# Yaliyomo


Tahadhari! Kama unahitaji msaada kwa lugha yako, tafadhali piga simu kwa 1-800-250-8427 ........ 2
Yaliyomo ........ 3
Karibu kwenye Mpango Wako wa Green Mountain Care ........ 5
Majina ya Mpango ........ 5
    Kadi Yako ya Green Mountain Care ........ 6
Huduma ya Afya na Rufaa ........ 6
    Mtoa Huduma ya Msingi (PCP) ........ 6
    Huduma za Baada ya Saa za Kazi ........ 6
    Wataalamu ........ 6
    Kama Daktari wako Hapokei Green Mountain Care ........ 6
    Uchunguzi wa Mara kwa Mara ........ 7
Medicaid na Dk. Dynasaur ........ 7
    Mambo ambayo Programu Yako Inashughulikia (Huduma Unazoweza Kupata) ........ 7
    Malipo ya pamoja ya Medicaid ........ 8
    Malipo ........ 8
    EPSDT ........ 9
    Kile Ambacho Mpango wako Haugharamii ........ 10
    Kupata Huduma Zinazogharamiwa na Medicaid na Programu za Dk. Dynasaur ........ 10
    Misamaha ........ 10
    Idhini ya Awali ........ 10
    Vifaa vya Matibabu vya Kudumu (DME) ........ 11
    Dawa na Idhini ya Awali ........ 12
    Usafiri wa Matibabu Usio wa Dharura ........ 12
    Dharura ........ 12
Unapotakiwa Kulipa ........ 13
    Ukipata Bili ........ 14
    Kama Una Bima Nyingine ........ 14
Haki na Wajibu Wako ........ 14
    Una haki ya ........ 14
Ulaghai, Uharibifu na Matumizi Mabaya - Kuiba au Kudanganya Ili Kupata Pesa za Medicaid? ........ 15
Wosia na Maagizo ya Mapema ........ 15

Uchangiaji wa Viungo....16

Kutoa Taarifa kwa Mtoa Huduma Wako wa Msingi (PCP)....16

Notisi ya Shughuli za Faragha.... 16

Hakikisho la Ubora....17

Ikiwa Hukubaliani na Uamuzi Tuliotoa.... 17

Malalamiko.... 22

Je, unahitaji Msaada**?**.... 22

Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Vermont Health Connect & Green Mountain Care.... 22

Ofisi ya Utetezi wa Huduma za Afya (HCA).... 22

Taarifa za Ziada.... 23

Mipango Mingine.... 23

Huduma za Mchana kwa Watu Wazima.... 23

Mpango wa Huduma za Wahudumu.... 23

Huduma Jumuishi za Watoto (CIS).... 23

Huduma Jumuishi za Watoto - Afua ya Mapema (CIS-EI).... 23

Huduma za Matunzo Binafsi ya Watoto.... 24

Kliniki za Watoto wenye Mahitaji Maalum ya Afya (CSHN).... 24

Machaguo ya Uangalizi.... 24

Huduma za Ulemavu wa Ukuaji.... 24

Mpango wa Msaada wa Kifedha.... 25

Ufadhili Rahisi wa Familia.... 25

Huduma za Uuguzi za Teknolojia ya Hali ya Juu.... 25

Huduma za Wahudumu wa Nyumbani.... 25

Kliniki Maalum.... 25

Huduma Maalum.... 25

Mpango wa Vermont wa Kugundua na Afua ya Mapema wa Kusikia.... 26

Afya ya Akili.... 26

Huduma kwa Wagonjwa wa Nje Ambao ni Watu Wazima.... 26

Huduma za Watoto, Vijana na Familia.... 26

Ukarabati wa Jamii na Matibabu.... 26

Huduma za Dharura.... 26

Mpango wa Majeraha ya Kiwewe cha Ubongo.... 27

Mpango wa Wanawake, Watoto wachanga na Watoto (WIC).... 27

## Karibu kwenye Mpango Wako wa Green Mountain Care

Sehemu ya kwanza ya kitabu hiki inakuambia mambo ya mipango yote ya Green Mountain Care.

Je, una maswali? Wapigie simu huduma kwa wateja wa Vermont Health Connect & Green Mountain Care kwa **1-800-250-8427**. Piga simu Jumatatu hadi Ijumaa, kuanzia saa 2 asubuhi (8:00 a.m) hadi saa 10:30 jioni (4:30 p.m.) (kunafungwa siku za sikukuu). Namba hii pia iko nyuma ya kadi yako ya Green Mountain Care.

Ikiwa ungependa kusitisha huduma yako ya Green Mountain Care, piga simu **1-800-250-8427**. **AU** tuma barua kwa:

DCF/Kitengo cha Huduma za Kiuchumi
ADPC
103 South Main Street
Waterbury, VT 05671-1500

Watoa huduma wa Green Mountain Care wanapaswa kukupa huduma bora za matibabu unazohitaji. Madaktari hawapaswi kukataa, au kupunguza huduma zinazohitajika kimatibabu. Watoa huduma wa Green Mountain Care lazima wafuate sheria za serikali kuu zinazopinga ubaguzi. Yaani hutatendewa tofauti kwa sababu ya asili yako.

### Majina ya Mpango

**Medicaid** ni huduma ya afya kwa watoto, wazazi, walezi na wazee. Medicaid pia inashughulikia watu wenye ulemavu wanaokidhi miongozo ya mpango. Na inashughulikia watu wazima wasio na watoto ambao wamekidhi kanuni fulani. Watu wengine wanaweza kupata huduma ya muda mrefu ya Medicaid. Ni lazima watimize kanuni za afya za Idara ya Ulemavu, Wazee na Maisha ya Uhuri. Ni lazima pia watimize kanuni za mapato na rasilimali.

**Dk. Dynasaur** ni bima ya Medicaid ya gharama ya chini au bila malipo kwa watoto, vijana wenye umri chini ya miaka 19, na wanawake wajawazito.

### Kadi yako ya Green Mountain Care

Kitambulisho chako kitatumwa nyumbani kwako. Tafadhali kionyeshe unapoenda kupata huduma ya afya.
Ikiwa hukupata kitambulisho chako kipya ndani ya mwezi mmoja baada ya kupata kijitabu hiki, **AU** umepoteza kadi yako? Piga simu **1-800-250-8427** na omba kadi mpya. Je, una bima nyingine ya afya? Unapaswa kumwonyesha mtoa huduma afya wako kadi zako zote za cha bima.

## Huduma ya Afya na Rufaa

### Daktari wako au Mtoa Huduma ya Msingi (PCP)

**Msingi** maana yake kwanza. Mtoa Huduma wako wa Msingi ndiye unayempigia simu kwanza unapohitaji huduma ya matibabu. Katika kijitabu hiki, tunamwita **daktari** wako. Watakupa huduma nyingi za afya yako. Daktari wako atashirikiana na wewe kuona mtaalamu kama unahitaji. Mtaalamu ni mtu ambaye hutoa aina moja tu ya huduma. Mifano: daktari wa moyo, daktari wa figo.

Je, daktari wako ni mgeni kwako? Muombe daktari wako wa zamani atume taarifa zako za matibabu kwa daktari wako mpya. Piga simu kwa daktari wako mpya kusema kwamba taarifa zinakuja. Ni muhimu kwa daktari wako kuwa na taarifa zako za matibabu.

### Huduma za Baada ya Saa za Kazi

Jaribu kuonana na daktari wako kwa matatizo ya kiafya wakati wa saa za kazi za kawaida. Ikiwa wewe ni mgonjwa kweli au unaumia ofisi ya daktari wako inapokuwa imefungwa piga simu kwa daktari wako na uombe msaada au ushauri.

Ofisi ya daktari wako itapokea simu saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Tazama **Dharura** kwenye ukurasa wa 12 kwa taarifa zaidi.

### Wataalamu

Mtaalamu ni mtu ambaye ana mafunzo ya ziada. Hushughulikia aina fulani za matatizo ya kiafya. Mfano: Kwa matatizo ya moyo, unahitaji mtaalamu wa moyo. Daktari wako atakusaidia kupata miadi. Hii inaitwa **rufaa**. Mara nyingi, lazima umuone daktari wako <u>kabla ya</u> kwenda kwa mtaalamu. Daktari wako anaweza kukusaidia kuamua ikiwa unahitaji mtaalamu. Anaweza kukusaidia kuchagua ni mtaalam yupi wa kumuona. Ikiwa unahitaji kuonana na mtaalamu ambaye hatumii Medicaid, lazima upate rufaa kutoka kwa daktari wako <u>kwanza</u>. Ikiwa hutafanya hivyo, huenda ukalazimika kulipia ziara hiyo.

## Ikiwa Daktari Wako Hapokei Green Mountain Care

Je, unamuona daktari asiyepokea Green Mountain Care? Unaweza kuendelea kumwona kwa hadi siku 60 <u>baada ya</u> kujiunga na mpango. Hii inaweza kutokea **IKIWA** tu**:**

- Una ugonjwa wa kutishia maisha **au**
- Una ugonjwa ambao unazidi kuwa mbaya au unakulemaza **au**
- Una mimba ya zaidi ya miezi 3 **na**

- Daktari anakubali kupokea malipo ya mpango na kufuata kanuni za mpango.

Unataka kuendelea kuonana na daktari wako kwa siku 60? Je, ungependa kujua zaidi kuhusu rufaa? Piga simu kwenye Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

Je, unataka kujua ni madaktari gani wanaotumia Green Mountain Care? Tumia zana ya Kutafuta Mtoa Huduma mtandaoni . Madaktari walioorodheshwa kuwa **nje ya mtandao** huenda wasipokee bima ya Green Mountain Care.

Daktari yeyote unayemwona lazima achukue Green Mountain Care. Wasipofanya hivyo, Green Mountain Care **haitawalipa**. Utalazimika kulipia huduma zao. Je, una bima nyingine ya afya ambayo inaweza kulipa gharama yote au sehemu ya gharama? Basi daktari wako lazima achukue zote Green Mountain Care na bima hiyo nyingine ya afya.

### Ikiwa Unahitaji Huduma Nje ya Mtandao wa Medicaid ya Vermont

Tuna mtandao mkubwa sana wa watoa huduma ikiwemo aina nyingi za wataalamu. Mtandao wetu umeundwa kushughulikia mahitaji anuwai ya matibabu. Wakati mwingine, mtandao huu hauwezi kutibu matatizo fulani maalum ya afya. Ikiwa unaamini unahitaji huduma za kibingwa ambao huwezi kuzipata kwa mtoa huduma wa Vermont Medicaid, wasiliana na PCP wako ili kujadili mahitaji yako. PCP wako anaweza kukuombea kibali cha wewe kupokea huduma kwa mtoa huduma ambaye si sehemu ya mtandao wetu ikiwa:

- Huduma unayohitaji ni ya lazima kiafya na unasimamiwa na Vermont Medicaid
- Mtoa huduma unayetaka kuona anakubali kufuata mahitaji yetu
- Tunaweza kubaini kwamba huduma unayohitaji haipatikani ndani ya mtandao wetu.

Hutatozwa zaidi kwa huduma zilizopatikana nje ya mtandao. Uidhinishaji wa huduma ya nje ya mtandao unahitajika.

### Uchunguzi wa Mara kwa Mara



Ni bora wakati wote kuzuia matatizo ya afya kabla hayajaanza. Uchunguzi wa mara kwa mara unaweza kusaidia. Muulize daktari wako mara ngapi ufanyiwe uchunguzi. Muulize daktari wako ni uchunguzi gani wa afya unahitaji kwa umri na afya yako.

## Medicaid na Dk. Dynasaur

### Je, Unaweza Kupata Huduma Gani?

Unaweza kupata ziara za daktari na mtaalamu, huduma ya hospitali, dawa, na huduma nyingine nyingi. Kuna sheria kuhusu aina na kiasi unachoweza kupata. Muone daktari wako kwanza kabla ya kuweka miadi na mtaalamu. Je, unahitaji huduma? Daktari wako anapaswa kuwapigia simu watoa Huduma kuhusu Huduma ili kuhakikisha kwamba huduma hiyo inagharamiwa kwa ajili yako. Huduma zinazogharamiwa ni:

- Huduma za hospitali za bila kulazwa - zinaitwa mgonjwa wa nje
- Huduma za dharura

- Upasuaji na kukaa hospitalini usiku kucha
- Mimba, uzazi, na huduma za watoto wachanga kabla na baada ya kuzaliwa
- Huduma za afya ya akili na matumizi ya dawa za kulevya, ikiwemo matibabu ya afya ya akili, ushauri nasaha na tiba ya kisaikolojia
- Dawa za kuandikiwa na daktari
- Huduma na vifaa vya urekebishaji na uboreshaji - kusaidia watu walio na majeraha, ulemavu, au tatizo la afya la kudumu au ujuzi wa kupona
- Huduma za maabara
- Huduma za kinga ili kulinda afya yako na huduma za kudhibiti magonjwa
- Huduma za meno, macho na kusikia
- Huduma na madaktari wa watoto (za watoto) na
- Usafiri = safari zisizo za dharura kwenda kwenye miadi ya matibabu

Je, una swali kuhusu huduma ambayo haijaorodheshwa? Piga simu kwenye Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

## Malipo ya pamoja ya Medicaid

- Wanachama wa Medicaid hulipa $3 kwa kila ziara ya daktari wa meno.
- Wanachama wa Medicaid hulipa $1, $2 au $3 kwa maagizo ya daktari.
- Wanachama wa Medicaid hulipa $3 kwa siku katika kila hospitali kwa ajili ya ziara za wagonjwa wa nje.

Baadhi ya huduma katika ofisi ya mtoa huduma nje ya hospitali bado ni huduma za wagonjwa wa nje wa hospitalini. Muulize mtoa huduma wako ikiwa huduma itatozwa kama “ziara ya wagonjwa wa nje wa hospitali.”
Ikiwa ni hivyo, malipo yako ya pamoja yatakuwa $3.

Watoto wengi, watu wenye ujauzito au mwaka mmoja baada ya kujifungua, na watu alio katika nyumba za malezi **hawapaswi** kulipa malipo ya pamoja. Watu walio katika Mpango wa Matibabu ya Saratani ya Matiti na Shingo ya Kizazi **hawalazimiki** kulipa malipo ya ushirika.

**Hupaswi** kulipa malipo ya ushirika kwa ajili ya:
- Huduma za kinga
- Huduma na vifaa vya uzazi wa mpango
- Huduma za dharura
- Huduma zinazohusiana na unyanyasaji wa kijinsia

## Malipo ya Bima

Baadhi ya Wanachama wa Dk. Dynasaur wanaweza kutakiwa kulipa malipo ya kila mwezi. Kiasi cha malipo kinategemea mapato, ukubwa na bima ya afya ya familia. Unapopata bili yako ya kwanza, lipa mara moja ili bima yako ianze kutumiaka. Endelea kulipa kwa wakati ili usipoteze huduma. Ukipoteza bili yako, wapigie simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427.** Wanaweza kukuambia ni kiasi gani unadaiwa na jinsi ya kulipa.

## EPSDT ni nini?

EPSDT ni Medicaid na Dk. Dynasaur kwa ajili ya watoto na vijana wenye umri wa miaka china ya 21. Inajaribu kuhakikisha kwamba watoto wanakuwa na afya bora kadri iwezekanavyo. **EPSDT** inasimamia Matibabu ya Uchunguzi wa Upimaji wa Mapema Katika Vipindi (Early Periodic Screening Diagnostic Treatment). Inapaswa:

- Kupata matatizo mapema, kuanzia kuzaliwa
- Jumuisha ziara za daktari wa uchunguzi kwa nyakati za kawaida zilizowekwa
- Kutumia vipimo vya uchunguzi ili kujua matatizo yoyote
- Kufanya vipimo vya ufuatiliaji ikiwa matatizo yanapatikana na
- Kutibu matatizo yoyote ya kiafya yanayopatikana

### Jinsi EPSDT Inafanya Kazi

EPSDT ni sheria ya serikali kuu. Inasema Jimbo **lazima** lilipie huduma yoyote ya afya inayohitajika. **Kuhitajika kiafya** maana yake ni kwa ajili ya tatizo hilo la kiafya. **NA** kwamba hivi ndivyo madaktari wengi wangefanya kutibu tatizo hilo. Linalipia huduma mbali na bima ya Medicaid kwa watu wazima. Hakuna ukomo wa huduma zinazohitajika kimatibabu. Baadhi ya huduma zinahitaji kuidhinishwa kabla ya kuzipata. Hii inaitwa idhini ya awali.

### EPSDT Inagharamia

- Uchunguzi wa mara kwa mara
- Vipimo vya jinsi mtoto au kijana anavyokua na anavyojifunza
- Sindano
- Vipimo vya macho
- Vipimo vya kusikia
- Uchunguzi wa sumu ya risasi
- Ziara za meno
- Ushauri
- Usafiri

### Je, ni mara ngapi mtoto huchunguzwa?

Kuna orodha ya vipimo vya afya ambavyo watoto na vijana wanapaswa kupata kila mwaka. Pia kuna orodha nyingine ya uchunguzi wa meno. Endelea kupata taarifa za kina na miongozo ya EPSDT.

### EPSDT hailipii:

- Huduma au bidhaa ambazo haziko katika sheria za serikali kuu za Medicaid (Kifungu cha 1905(a) cha Sheria ya Usalama wa Jamii).

- Huduma ya majaribio ambayo si salama au haifanyi kazi.
- Huduma au bidhaa za gharama kubwa au kama za bei nafuu zitafanya kazi vilevile.
- Huduma ambazo si za kimatibabu.

Kwa maelezo zaidi, tembelea ukurasa wa taarifa za wanachama wa Vermont Medicaid au piga simu **1-800-250-8427**.

### Kile Ambacho Mpango Wako Haugharamii

- Majeraha yanayohusiana na kazi ambayo yanapaswa kulipiwa na Fidia ya Mfanyakazi
- Gharama za huduma zilizoagizwa na mahakama isipokuwa kama zinahitajika kimatibabu pia
- Huduma ambazo hazijajaribiwa hapo awali au ni za majaribio
- Huduma za kuboresha jinsi unavyoonekana (huduma za vipodozi)
- Huduma ambazo hazihitajiki kiafya
- Tiba ya acupuncture, acupressure, au masaji
- Huduma zinazokusaidia kupata ujauzito (matibabu ya uzazi)
- Uanachama wa klabu za afya na
- Huduma katika nchi za nje

## Kupata Huduma Zinazogharamiwa na Medicaid na Programu za Dk. Dynasaur

### Ikiwa huduma haigharamiwi na Medicaid

Huduma zote zinazohitajika za kimatibabu zinagharamiwa na EPSDT kwa mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 21.
Je, itakuwaje kama huduma hailipiwi na Medicaid kwa watu wazima wenye umri wa miaka 21 na zaidi? Unaweza kutuomba tukulipie huduma hiyo. Huu huitwa **msamaha**. Kituo cha Huduma kwa Wateja kinaweza kukusaidia kuomba hili. Wewe na daktari wako mtapaswa kutuambia kuhusu huduma hizo na kwa nini unazihitaji. Tutakutumia jibu kwa njia ya barua ndani ya takriban siku 30.

Je, ungependa kujua zaidi au kuomba msamaha? Piga simu kwenye Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**. Fomu ziko katika ukurasa wa taarifa za msamaha wa bima kwa wanachama.

### Idhini ya Awali

Baadhi ya huduma na dawa zinahitaji kuidhinishwa kabla ya kuzipata. Hii inaitwa **idhini ya awali**. Madaktari wako wanajua huduma na dawa hizo ni zipi. Wataomba idhini ya awali itolewe kwa ajili yako.

Ikiwa tutapata taarifa zote tunazohitaji, idhini ya awali huamuliwa ndani ya siku 3. Wewe na daktari wako mtapata barua ya kukujulisha kuhusu uamuzi. Huna **haja ya** idhini ya awali kwa huduma za dharura.

## Vifaa vya Matibabu vya Kudumu (DME)

**Vifaa vya Matibabu vya Kudumu** ni vitu vya kukusaidia kurahisisha maisha na matibabu yako. Mifano ni viti vya magurudumu na vitanda vya hospitali.

### Je, ninapataje Vifaa vya Matibabu vya Kudumu?

**1. Daktari wako atakupeleka kwa mtu kwa ajili ya vipimo.**

- Vipimo huamua aina ya kifaa unayohitaji. Hii inaitwa **tathmini**. Tathmini nyingi hufanywa na wataalam wa mazoezi au masuala ya utendaji. Watapanga muda wa kukutana nawe. Huenda ukasubiri kama wana shughuli nyingi. Huenda ukahitaji kusubiri kama unahitaji kujaribu kifaa kwanza.
- **Kumbuka:** Je, vifaa unavyohitaji ni rahisi? Daktari wako anaweza kusema hauhitaji tathmini. Ikiwa ndivyo, ruka hadi hatua ya 2.
- Watatuma fomu kwa daktari wako. Itaonyesha ni aina gani ya vifaa unahitaji.

**2. Daktari wako ataandika maelezo.**

- Daktari wako atasaini fomu ya tathmini na kuandika maagizo. Watatuma agizo lako kwenye kampuni ya Vifaa vya Matibabu vya Kudumu ambayo ina vifaa hivyo.

**3. Kampuni ya Vifaa vya Matibabu vya Kudumu itaomba Medicaid idhini ya awali.**

**Iwapo HUHITAJI idhini ya awali, ruka hadi hatua ya 5.**

- Je, unahitaji idhini ya mapema? Kampuni ya DME itatuma taarifa za Medicaid zinazokuhusu wewe na DME unayohitaji. **Idhni ya awali** inamaanisha kwamba Medicaid lazima iseme ni sawa kabla ya kupata kifaa.
- Mkaguzi ataangalia taarifa zako. Wataamua kama una hitaji la kimatibabu la kifaa.
- Ikiwa mkaguzi anahitaji taarifa za zaidi, Medicaid itaomba kampuni ya DME iyatume. Medicaid ina siku 14 kuanzia ombi la kwanza la kufanya uamuzi.

**4. Medicaid watakuambia wanachoamua**

- Medicaid itakutumia barua wewe, mtoa huduma wako, na kampuni ya DME. Barua hiyo inaitwa Notisi ya Uamuzi. Katika jimbo la Vermont, Idara ya Upatikanaji wa Afya ya Vermont (DVHA) inaendesha Medicaid. Barua hizo zitatoka DVHA.

**5. Kampuni ya DME itachukua vifaa kwa ajili yako**

Medicaid ikiidhinisha, kampuni ya DME itakupa au itaagiza vifaa.

Ikiwa Medicaid **haitaidhinisha** , unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo. Ili kukata rufaa, piga simu kwenye Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**. **Rufaa** inawaomba waangalie kesi yako tena. Medicaid hufanya jitihada kuidhinisha maombi ya Vermont DME

haraka. Kwa viti vya magurudumu vyenye muundo tata, huchukua kama siku 9. Hiyo ni haraka kuliko kanuni za Medicaid zinavyotaka. Pia, ni haraka kuliko majimbo mengine mengi. Kwa vifaa rahisi, muda ni haraka zaidi. Je, una Medicaid na Medicare au mpango mwingine wa bima? Basi inaweza kuchukua muda mrefu zaidi.

## Dawa na Idhini ya Awali

Green Mountain Care inawaomba madaktari kuagiza dawa kutoka kwenye orodha ya dawa zilizochaguliwa. Hii husaidia kupunguza gharama. Baadhi yake ni dawa za kawaida/za jenasi ambazo ni gharama ndogo. Zinafanya kazi sawa na dawa za chapa zenye gharama kubwa. Madaktari na maduka ya dawa lazima yakupe dawa ya bei ya chini ambayo itakusaidia. Je, ikiwa unakataa dawa ya kawaida/ya jenasi na unataka chapa yenye jina? Huenda ukalazimika kulipia mwenyewe dawa ya chapa yenye jina.

Baadhi ya dawa unaweza kupewa kwa matumizi ya siku 90. Zinajumuisha dawa za shinikizo la damu, lehemu na ugonjwa wa kisukari. Mara ya kwanza unapojaribu dawa, unaweza kupata dawa chache. Hii inakuwezesha wewe na daktari wako kuamua kama zinakufaa. Baada ya hapo, utapata dawa za siku 90.

Vipi kama daktari wako anadhani unahitaji dawa ya chapa yenye jina? Au anadhani huhitaji dawa za siku 90? Wanaweza kutuomba tulipe dawa hiyo. Je, unataka nakala ya orodha ya dawa unazopendelea? **AU** orodha ya dawa zinazohitaji kutumika siku 90? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**. Au tazama orodha ya dawa unazopendelea mtandaoni.

## Usafiri wa Matibabu Yasiokuwa ya Dharura

Safari za kwenda kwenye miadi na huduma za matibabu zisizo za dharura zinapatikana kwa wanachama hao wa Medicaid ambao hawana usafiri na hawaishi kwenye njia ya basi la umma. Miadi inahitaji kuwa ya kwenda kwa mtoa huduma wa Medicaid, na unapaswa kulipiwa na Medicaid. Safari za kuchukua dawa pia zimejumuishwa.

Mifano ya usafiri unaopatikana ni pamoja na kumiliki gari lililosajiliwa na lenye bima; wanafamilia wa karibu wanaomiliki magari; safari zinazotolewa na magari yanayomilikiwa na kituo; na usafiri wa umma unaopatikana kwa urahisi.

Kwa maswali na/au kupanga safari, tafadhali wasiliana na Chama cha Usafiri wa Umma cha Vermont kwa **1-833-387-7200**.

## Dharura

Dharura ni ugonjwa wa ghafla na usiotarajiwa, tatizo la kiafya, au tatizo la afya ya akili, yenye dalili ambazo unaamini zinaweza kuwa tishio kubwa kwa afya au maisha yako ikiwa hautapata matibabu haraka. DVHA haiweki mipaka au haifasili kile unachofikiri ni dharura. Hii ni baadhi ya mifano, lakini dharura sio tu orodha hii:

- Maumivu ya kifua
- Mifupa iliyovunjika

- Degedege au kifafa
- Kutokwa na damu nyingi
- Kuungua sana
- Maumivu makali
- Tatizo la afya ya akili

DVHA haitazuia malipo ikiwa utaelekezwa kutafuta huduma ya dharura. Huduma za dharura na huduma za baada ya uimarishaji hulipwa kwa walengwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki.

Huduma za baada ya dharura ili kuhakikisha kuwa afya yako ni thabiti baada ya dharura pia hulipiwa.

Huduma za matibabu ya dharura kama vile kushonwa, upasuaji, eksirei, au taratibu zingine, pia hulipiwa.

Ikiwa una dharura, piga simu 911 au nenda kwenye chumba cha dharura kilicho karibu au hospitali kwa huduma ya dharura mara moja. Huna haja ya rufaa kutoka PCP wako kupata huduma ya dharura. Mjulishe PCP wako kilichotokea haraka uwezavyo.

Ikiwa unahitaji huduma ya dharura unaposafiri nje ya mtandao wa Green Mountain Care, piga simu 911 au nenda kwenye idara ya dharura iliyo karibu nawe haraka. Green Mountain Care inawajibika kulipia huduma ya dharura. Pia, tunawajibika kulipia huduma inayohitajika ili kuimarisha afya yako baada ya huduma ya dharura kutolewa.

Unapoweza kufanya hivyo, wasiliana na Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa 1-800-250-8427 ili utuambie kuhusu huduma yako ya dharura. Unapaswa pia kuipigia namba hii ikiwa utapokea bili ya huduma yako. Tutashirikiana na mtoa huduma kufuata kanuni zinazohitajika ili tulipie huduma yako.

## UNapotakiwa Kulipa

Ikiwa hutafuata sheria za mpango, huenda ukalazimika kulipia huduma mwenyewe. Hii inaweza kutokea **IKIWA:**

- Unahitaji rufaa au idhini ya awali kabla ya kupata huduma na hujaipata; **AU**
- Unaenda kwa mtoa huduma ambaye hachukui Green Mountain Care; **AU**
- Mtoa huduma wako anakuambia huduma haijumuishwi, na unaipata hata hivyo.

Hakikisha unamwambia mtoa huduma wako kuwa uko kwenye Green Mountain Care. Watakuambia ikiwa hawatakubali bima yako.

Je, hutaki kupata bili za matibabu yako? Fuata sheria za mpango wako.

### Ukipata Bili

- Fungua bili mara moja,

- Piga simu kwa mtoa huduma na uhakikishe kuwa anajua uko kwenye Green Mountain Care, na
- Piga Simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427** kupata msaada.
- **Usilipe bili kabla ya kupiga simu Huduma kwa Wateja.** Green Mountain Care inaweza kuwalipa watoa huduma pekee. Ukilipa, hatuwezi kukurudishia pesa yako.

## Kama Una Bima Nyingine

Kama una bima nyingine, fuata kanuni zao. Nenda kwa madaktari walio katika mpango wako wa bima na katika mipango yetu. Daktari wako lazima atoze bima yako nyingine kwanza. Mipango yetu inaweza kusaidia kulipa kile ambacho bima yako nyingine hailipii.

## Haki na Wajibu Wako

### Una haki ya

- Kutendewa kwa adabu,
- Kutunzwa kwa uangalifu,
- Kuchagua na kubadilisha daktari/watoa huduma wako,
- Kupata ukweli kuhusu huduma za mpango wako na daktari/watoa huduma,
- Kuambiwa kuhusu afya yako kwa maneno ambayo unaweza kuyaelewa,
- Kuamua kuhusu huduma yako ya afya, kujibiwa maswali yako, na kukataa matibabu,
- Kuuliza na kupata nakala ya taarifa zako za matibabu. Unaweza kuomba mabadiliko kama taarifa si sahihi,
- Pata maoni ya pili kutoka kwa daktari/mtoa huduma mwenye sifa aliyejiandikisha katika Vermont Medicaid,
- Kuzungumza kuhusu mpango wako au maswala ya huduma ya afya (tazama ukurasa wa 20),
- Kutozuiliwa au kutotengwa kwa sababu ya uonevu, adhabu, au kwa sababu ni rahisi zaidi,
- Omba rufaa ikiwa umenyimwa huduma unazofikiri unahitaji. Tazama ukurasa wa 19 kwa maelezo zaidi.

### Unapaswa kutunza afya yako kwa:

- Kumwambia daktari wako kuhusu dalili zako za ugonjwa na historia ya afya,
- Kuuliza maswali unapohitaji kujua zaidi au unapokuwa huelewi kitu,
- Kufuatia mipango ya matibabu ambayo wewe na daktari wako mnakubali,
- Kutekeleza miadi yako au kupiga simu mapema ili kughairi kama huwezi kufika,
- Kufahamu kuhusu kanuni za mpango wako ili utumie huduma bora uwezavyo,
- Kuhakikisha kuwa una rufaa kutoka kwa daktari/PCP wako (inapohitajika) kabla ya kuwaona watoa huduma wengine,
- Kulipa malipo ya bima na malipo ya ushirikiano kama inavyohitajika,
- Kupiga simu ili kughairi au kupanga upya ikiwa huwezi kwenda kwenye miadi

# Udanganyifu, Uharibifu, na Dhuluma

**Je, Kuna Mtu Anaiba au Anadanganya ili Kupata Pesa za Medicaid?**
Kiambie Kitengo Maalum cha Uchunguzi. Hivi ndivyo jinsi ya kuwafikia:

- **Tovuti:** Fomu ya Rufaa ya Ulaghai na Dhuluma
- **Barua pepe:** **ReportMedicaidFraud@vermont.gov**
- **Simu:** 802-241-9210
- **Faksi:** 802-871-3090 (faksi ya moja kwa moja kwenda "Kitengo Maalum cha Uchunguzi cha DVHA")
- **Anwani ya Posta:**

  Kitengo Maalum cha Uchunguzi cha DVHA
  NOB 1 South, 280 State Drive
  Waterbury, VT 05671-1010

# Wosia na Maagizo ya Mapema

**Wosia** ni taarifa ya maandishi. Unasema:

- Je, ni nani anayeweza kukufanyia maamuzi ya kiafya unapokuwa huwezi,
- Ni kiasi gani mtu anaweza kuamua,
- Daktari/mtoa huduma wako wa msingi ni nani,
- Ni huduma gani za afya na au matibabu unayotaka,
- Jinsi unavyotaka masuala binafsi yashughulikiwe, kama vile mazishi yako,
- Nani unayemtaka kuwa mlinzi wako, ikihitajika,
- Nani **usiyemtaka** kufanya maamuzi kwa ajili yako
- Unataka uangalizi wa aina gani kama unakufa

Wosia ni bure. Pia huitwa mwongozo wa mapema au mamlaka ya kudumu ya uwakilishi kwa huduma ya afya. Zinaweza kuitwa hati ya uangalizi wa mwisho wa maisha. Sheria ya Vermont kuhusu wosia ni sheria ya Maagizo ya Mapema ya Vermont (Andiko la 18, Sura ya 231).

Unaweza kuwa mgonjwa sana kiasi cha kushindwa kufanya maamuzi ya afya. Ikiwa **hakuna** dharura, Madaktari hawawezi kukupa huduma papo hapo. Ni lazima kwanza wajue kama una wosia. Ikiwa unao, lazima watii maelekezo katika wosia. **AU** watii maelekezo ya mtu uliyemchagua kufanya maamuzi ya afya.

Je, daktari anaweza kukataa kufuata maelekezo katika maagizo yako ya mapema? Ndiyo, ikiwa imani zao za kimaadili au za kitaratibu zinawafanya waamini kuwa ni makosa. **LAKINI** lazima:

- Wakwambie wewe na mtu uliyemtaja kufanya maamuzi;
- Kusaidia kuhamisha huduma yako kwa daktari mwingine ambaye atatii maelekezo;
- Kuendelea kukupa huduma za afya hadi daktari mpya apatikane; na
- Kueleza katika taarifa yako ya matibabu:
  - tatizo
  - hatua zilizochukuliwa ili kuirekebisha na
  - jinsi tatizo lilivyotatuliwa.

Kila mhudumu wa afya lazima atii sheria ya wosia. Ni lazima wawe na kanuni zao ili kuhakikisha sheria na kanuni zinafuatwa.

Je, unafikiri kuna mtu hafuati sheria? Piga simu kwenye Idara ya Leseni na Ulinzi kwa **1-800-564-1612. AU** nenda mtandaoni ili kuwasilisha malalamiko. **AU** tuma barua kwa:

Idara ya Leseni na Ulinzi
103 South Main Street, Ladd Hall
Waterbury, VT 05671

Je, unataka taarifa kuhusu sheria ya nchi na wosia? Piga simu kwenye Mtandao wa Maadili wa Vermont kwa **1-802-828-2909. AU** nenda kwenye tovuti yao. Pia wana fomu za kuandaa wosia.

Andiko la 18 ni sheria ya Vermont kuhusu wosia. Unataka kujua zaidi? Zungumza na daktari wako au piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

## Uchangiaji wa Viungo

Unaweza kutaka kutoa ufadhili wa viungo vyako unapokufa. Mchangiaji mmoja anaweza kusaidia watu wengi. Ili kupata maelezo zaidi, piga simu kwa **1-888-275-4772** kwa taarifa bila malipo.

## Kutoa Taarifa kwa Daktari/PCP wako

Tunaweza kumpa daktari wako orodha yenye jina lako. Hii ni kumsaidia daktari wako kukupa huduma ya afya unayohitaji. Baadhi ya orodha hizi zinaweza kuwa kuhusu:

- Wagonjwa wenye ugonjwa wa kisukari ambao hawajachunguzwa macho yao mwaka jana,
- Wanawake ambao hawajapata kipimo cha pap au mammogram hivi karibuni,
- Watoto ambao hawajachanjwa chanjo zao mpya,
- Dawa zinazoweza kutoa athari mbaya zinapochanganywa na dawa nyinginezo, na
- Watoto ambao wako nyuma kwenye vipimo vyao vya kawaida.

## Notisi ya Shughuli za Faragha

Umepokea barua inayosema kuwa umetimiza sheria za programu zetu. Pia ilikuwa na nakala ya **Notisi yetu ya Shughuli za Faragha.** Sheria ya serikali kuu, inayoitwa HIPAA, inasema lazima tukupe notisi. Notisi inakuambia haki zako za faragha. Inasema jinsi taarifa zako za afya zinavyoweza kutumiwa au kutolewa. Je, unahitaji nakala nyingine ya notisi? Piga Simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427** na uiombe. **AU** unaweza kuiona mtandaoni.

Je, unahisi taarifa zako hazijawekwa kwa usiri? Piga simu kwa Afisa wa Faragha wa AHS kwa **802-241-2234. AU** tembelea ukurasa wa malalamiko ya taarifa za afya.

## Mpango wa Hakikisho la Ubora

Huu ni mpango wa kuhakikisha kwamba unapata uangalizi bora wa afya na huduma bora. Baadhi ya mambo tunayoangalia ili kuhakikisha ni:

- Wagonjwa wanatumia dawa kiasi gani,
- Ni wanachama wangapi wanapata huduma ya mara kwa mara ili kuzuia magonjwa,
- Ni wanachama wangapi wanaotumia chumba cha dharura wakati **hakuna** dharura,
- Jinsi wahudumu wa afya ya mwili na akili wanavyofanya kazi pamoja,
- Jinsi wanachama na watoa huduma wanafurahishwa na programu zetu.

Tunawaomba madaktari kufuata miongozo yetu bora ya mazoezi kwa magonjwa fulani sugu. Hii inaweza kukufanya uwe na afya njema.

Je, kuna njia ambazo tunaweza kuboresha mipango yetu na kuifanya ikufanyie kazi vizuri zaidi? Piga Simu Huduma kwa Wateja **1-800-250-8427**. Maoni yako yatakuwa sehemu ya ukaguzi wetu wa ubora.

## Nini cha Kufanya Unapokuwa Hukubaliani na Uamuzi Tuliofanya

Unaweza kukata rufaa. Hii inamaanisha kumuomba mtu aangalie kesi yako. Watachunguza kuona kama tulifanya makosa. Endelea kusoma ili kujua zaidi.

Amua kile unachokatia rufaa.

- Je, unakata rufaa ya malipo ya lazima?
- **AU** unata rufaa kuona kama unaweza kupata au kuendelea na
    - Medicaid/Dk. Dynasaur,
    - VPharm, au
    - Mpango wa Akiba wa Medicare?

**Kama ndiyo**, tazama hapa chini "Ikiwa hukubaliani na uamuzi wetu wa kustahiki."

- Je, unakata rufaa kwa sababu Medicaid/Dk. Dynasaur haikulipia huduma?
    - **Ikiwa ndiyo,** tazama hapa chini "Ikiwa hukubaliani na uamuzi kuhusu huduma zako za afya."

### Ikiwa hukubaliani na uamuzi wetu wa kustahiki

**Omba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo.** Afisa anayesikiza shauri katika Bodi ya Huduma za Binadamu atasikiliza kesi yako. Ataamua ikiwa Vermont Medicaid ilifanya uamuzi sahihi.

**Una siku 90 za kuomba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo.** Angalia barua ya notisi iliyokukataza. Siku 90 huanza tarehe ya barua hiyo.

Kuna **njia 3** za kuomba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo:

1. **Wapigie Simu** Huduma kwa Wateja kwa 1-800-250-8427.
2. **Mtandaoni** nenda kwenye ukurasa wa rufaa kwenye intaneti. Ikiwa una akaunti ya mtandaoni ya VHC, fomu ya rufaa iko ndani ya akaunti yako.
3. **Tuma barua** kwa:

   Bodi ya Huduma za Binadamu<br>14-16 Baldwin St., 2nd Floor<br>Montpelier, VT 05633-4301

Katika barua au barua pepe, andika jina lako, tarehe ya kuzaliwa, na namba ya simu. Sema unachokatia rufaa na kwa nini.

**Je, tulisimamisha Medicaid/Dk. Dynasaur, VPharm au Mpango wa Akiba wa Medicare?** Unaweza kuendelea nazo wakati wa Usikilizaji wako wa Shauri la Haki katika Jimbo. Hii tunaiita "mwendelezo wa mafao." Tazama **Kuendelea na Huduma ya Afya Wakati Unakata Rufaa - Mambo Mengine Unayopaswa Kujua** hapa chini.

Lazima uombe hii ndani ya siku 11 kuanzia tarehe ya notisi. **AU** kabla ya mabadiliko kuanza, chochote kinachokuja **baadae**. Siku 11 zinaanza tarehe ambayo Vermont Medicaid ilikutumia uamuzi wake. Hii ni tarehe ya muhuri wa posta. Ni lazima ulipe malipo yako kwa wakati unaofaa wakati wa rufaa yako. Usipofanya hivyo, huduma yako ya afya inaweza kufikia mwisho. Ili kuendelea kupata huduma za afya wakati wa rufaa yako, piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.
**Je, unakata rufaa ni kiasi gani cha malipo yako ya bima?** Lazima ufanye malipo yako kwa wakati. Usipofanya hivyo, bima yako inaweza kuisha. Je, vipi ikiwa unalipa kuzidi kiwango? Ukishinda Shauri lako la Haki katika Jimbo, tutakulipa.

## Nini kitatokea unapoomba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo?

Vermont Medicaid itaangalia kesi yako tena. Hii inaweza kuchukua hadi siku 15. Mtu katika Timu ya Rufaa ya Huduma ya Afya atazungumza nawe kuhusu rufaa yako. Huenda tukaweza kutatua tatizo lako bila Shauri la Haki katika Jimbo.

Je, ikiwa **hatuwezi** kubadili uamuzi wetu? Basi tutaiambia Bodi ya Huduma za Binadamu unataka Shauri la Haki katika Jimbo. Utapata barua kutoka kwao. Afisa anayesikiza shauri ni mtu ambaye ataamua kesi yako. Wataweka mkutano wa kusikiliza upande wako. Wataamua ikiwa Vermont Medicaid ilifanya makosa. Unapaswa kwenda kwenye mkutano huu. Unaweza kujisemea mwenyewe au kuwa na mwakilishi.

**Itachukua muda gani?** Ni lazima waamue kesi yako **ndani ya siku 90** tangu tarehe uliyokata rufaa mara ya kwanza.

**Je, unahitaji uamuzi wa haraka zaidi?** Tuambie ikiwa kusubiri kutaumiza sana afya au maisha yako. Ukitimiza kanuni hizo unaweza kupata Usikilizaji wa haraka (yanayoharakishwa). Je, unapata Medicaid kwa sababu wewe ni kipofu, mlemavu, au una miaka 65 au zaidi? Basi tutaamua **haraka iwezekanavyo**. Je, unapata Medicaid kwa sababu nyingine? Basi utapata uamuzi **ndani ya siku 7**.

### Ikiwa hukubaliani na uamuzi kuhusu huduma zako za afya

#### Omba Rufaa ya Ndani ya Nyumba (ya Ndani)

Mtu wa Vermont Medicaid ataangalia kesi yako na kufanya uamuzi mpya. Itakuwa ni mtu ambaye hakuwa sehemu ya kufanya uamuzi wa kwanza. Mara nyingi, lazima ukate rufaa ya ndani kwanza. Ikiwa bado hukubaliani, unaweza kuomba Usikilizaji wa Haki katika Jimbo.

Una **siku 60** za kuomba rufaa ya ndani. Siku 60 zinaanza siku ambayo Vermont Medicaid ilikutumia taarifa ya uamuzi. Daktari/mtoa huduma wako anaweza kuomba rufaa ikiwa unataka.

**Kuna njia 3 za kuomba rufaa ya ndani:**

1. **Piga simu** Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427.** TDD/TTY: 1-888-834-7898
2. **Mtandaoni:** Taarifa za Mwanachama za Rufaa na Usikilizaji wa Haki **AU Tuma barua pepe** AHS.DVHAHealthCareAppealsTeam@vermont.gov
3. **Tuma barua** kwa:

   Idara ya Upatikanaji wa Afya ya Vermont
   Timu ya Rufaa za Huduma ya Afya
   150 Pilgrim Park – 3rd Floor
   Waterbury, VT 05671-4030

Katika barua au barua pepe, andika jina lako, tarehe ya kuzaliwa, na namba ya simu. Sema unachokatia rufaa. Sema ni huduma gani ulizoomba na ikiwa ulinyimwa.

**Je, tulipunguza au kusimamisha huduma za afya ambazo tayari unapata?** Unaweza kudumisha huduma zako wakati wa rufaa yako. Lazima uulize hii kabla ya huduma kuisha. Hii tunaiita "mwendelezo wa mafao." Tazama **Kuendelea na Huduma ya Afya Wakati Unakata Rufaa - Mambo Mengine Unayopaswa Kujua** hapa chini.

Ni njia ipi bora ya kuendelea kupata huduma zako? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

**Nini kinatokea katika rufaa ya ndani?** Vermont Medicaid itaweka mkutano ili kupata taarifa zaidi. Unapaswa kushiriki katika mkutano huu. Unaweza kujisemea mwenyewe au kuwa na mwakilishi. Daktari/mtoa huduma wako anaweza kuzungumza au kutoa taarifa kwa Vermont Medicaid.

**Mara nyingi, Vermont Medicaid lazima iamue rufaa yako ndani ya siku 30**. Je, itakuwaje ukiomba muda zaidi? Je, itakuwaje ikiwa kusubiri kwa muda mrefu kunaweza kukusaidia? Mifano: Daktari wako anahitaji muda zaidi kutuma maelezo. Au huwezi kufika kwenye mkutano wakati huo. Basi inaweza kuchukua siku 14 zaidi . Muda mrefu zaidi ambao uamuzi utawahi kuchukua ni **siku 44**.

**Je, unahitaji Vermont Medicaid ili kuamua rufaa yako kwa haraka zaidi?** Tuambie ikiwa kusubiri kutaumiza sana afya au maisha yako. Vermont Medicaid itaona kama unatimiza sheria za kukata rufaa haraka (kuharakishwa). Ukifanya hivyo, utapata uamuzi **ndani ya saa 72**. Inaweza kuchukua muda mrefu ikiwa utaomba hii au inaweza kukusaidia. Muda mrefu zaidi wa rufaa ya haraka inaweza kuchukua ni **siku 17**.

**Una haki ya kujua jinsi tulivyoamua rufaa yako.** Unaweza kuona karatasi, sheria, na uthibitisho tuliotumia. Unaweza kuona jinsi tulivyoamua ikiwa ulichoomba ni muhimu kiafya. Unaweza kupata nakala za karatasi hizi zote bila malipo. Ili kuomba nakala, pigia Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

**Je, unahitaji ushauri wa kisheria au msaada mwingine?** Unaweza kupata msaada bila malipo kutoka kwenye Msaada wa Kisheria wa Vermont. Piga simu Ofisi yao ya Utetezi wa Huduma za Afya kwa **1-800-917-7787**. **AU** nenda kwenye tovuti yao kwenye intaneti. Jaza fomu.

**Iwapo Hukubaliani na Uamuzi wa Rufaa ya Ndani**

Unaweza kuomba Usikilizaji wa Haki katika Jimbo. Afisa anayesikiza shauri katika Bodi ya Huduma za Binadamu atasikiliza kesi yako. Ataamua ikiwa Vermont Medicaid ilifanya uamuzi sahihi.

Mara nyingi, rufaa ya ndani lazima iwe ya kwanza. Kisha unaweza kuomba Usikilizaji wa Haki katika Jimbo. Je, itakuaje ikiwa Vermont Medicaid haitaamua rufaa yako ya ndani kwa tarehe yake ya mwisho? Basi unaweza kuomba masikizo ya Haki ya Jimbo bila kusubiri uamuzi. Muda mrefu zaidi rufaa yako ya ndani inaweza kuchukua ni:

- Siku 30 kwa rufaa ya ndani **AU**
- Siku 44 ikiwa wewe au sisi tuliomba muda zaidi kwa sababu kuchelewa kunaweza kukusaidia **AU**
- Saa 72 kwa rufaa ya haraka **AU**
- Siku 17 za kukata rufaa ya haraka **ikiwa** wewe au sisi tuliomba muda zaidi

Una **siku 120** za kuomba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo. Je, siku 120 zinaanza lini? Kwa tarehe ya barua inayokuambia uamuzi wa rufaa ya ndani.

**Kuna njia 3 za kuomba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo:**

1. Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427.** TDD/TTY: 1-888-834-7898.
   **AU** piga simu kwenye Bodi ya Huduma za Binadamu kwa **802-828-2536.**
2. **Mtandaoni kwenye tovuti ya Bodi ya Huduma za Binadamu**
3. Tuma barua kwa:

Bodi ya Huduma za Binadamu
14-16 Baldwin St., 2nd Floor
Montpelier, VT 05633-4301

Katika barua, andika jina lako, tarehe ya kuzaliwa na namba ya simu. Sema unachokatia rufaa. Sema ni huduma gani ulizoomba na ikiwa ulinyimwa.

**Je, tulipunguza au kusimamisha huduma za afya ambazo tayari unapata?** Unaweza kudumisha huduma zako wakati wa Usikilizaji wa Shauri lako la Haki katika Jimbo. **LAKINI** ni lazima uombe hili **ndani ya siku 11** za uamuzi wa rufaa ya ndani. Siku 11 zinaanza kuanzia tarehe ambayo Vermont Medicaid ilikutumia uamuzi wake wa kukata rufaa. Je, tayari uliomba kuendelea na huduma zako wakati wa rufaa ya ndani? Inabidi uombe tena. Hii tunaiita "mwendelezo wa mafao." Tazama **Kuendelea na Huduma ya Afya Wakati Unakata Rufaa - Mambo Mengine Unayopaswa Kujua** hapa chini.

Ni njia ipi bora ya kuendelea kupata huduma zako? Piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

**Nini kitatokea unapoomba Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo?** Utapata barua kutoka Bodi ya Huduma za Binadamu. Afisa anayesikiza shauri ni mtu ambaye ataamua kesi yako. Wataweka mkutano wa kusikiliza upande wako. Wataamua ikiwa Vermont Medicaid ilifanya makosa. Unapaswa kushiriki katika mkutano huu. Unaweza kujisemea mwenyewe au kuwa na mwakilishi.

**Itachukua muda gani kupata uamuzi kuhusu Shauri lako la Haki katika Jimbo?** Bodi ya Huduma za Binadamu lazima iamue kesi yako **ndani ya siku 90.** Siku 90 zinaanza tarehe uliyoomba kukata rufaa ya ndani kwa mara ya kwanza. Siku ulizotumia kuomba Usikilizaji wa Shauri baada ya uamuzi wa rufaa **hazihesabiwi**.

**Je, unahitaji uamuzi wa haraka zaidi?** Tuambie ikiwa kusubiri kutaumiza sana afya au maisha yako. Je, unakidhi kanuni za Usikilizaji wa Shauri la Haki katika Jimbo kwa haraka? Basi utapata uamuzi **ndani ya siku 3 za kazi**.

### Kuendelea na Huduma ya Afya Wakati Unakata Rufaa - Mambo Mengine Unayopaswa Kujua

- Je, ulilipia huduma mwenyewe? Ukishinda rufaa au kesi, huenda tukalazimika kukulipa.
- Je, uliendelea na huduma zako wakati wa kukata rufaa? Ukipoteza, **huenda** ukalazimika kulipia huduma ulizopata wakati wa kukata rufaa.
- Je, unaomba rufaa au usikilizaji wa shauri? Wakati huohuo, unaweza kuomba kuendelea na huduma hadi shauri linapoisha.
- Je, rufaa yako au shauri lako ni kuhusu huduma iliyoisha au iliyositishwa? Je, iliisha au ilikatwa kwa sababu ya mabadiliko ya sheria ya serikali kuu au jimbo? Ikiwa ndivyo, **huwezi kuendelea** na huduma wakati wa rufaa au usikilizaji wa shauri.

## Je, unahitaji ushauri wa kisheria au msaada mwingine kuhusu rufaa yako?

Unaweza kupata msaada **bila malipo** kutoka kwenye Msaada wa Kisheria wa Vermont. Piga simu kwenye Ofisi yao ya Utetezi wa Huduma za Afya kwa **1-800-917-7787. AU** nenda kwenye tovuti yao kwenye intaneti. Jaza fomu.

## Aina zingine za malalamiko kuhusu huduma zako za afya - unaweza kuwasilisha malalamiko

Je, hufurahishwi na mahali au wakati unaopaswa kwenda kupata huduma? Je, unafikiri huduma zako si nzuri vya kutosha? Je, ulidhurika baada ya kutumia haki zako? Haya ni mambo ambayo **huwezi kuyakatia rufaa**. Lakini unaweza kuwasilisha malalamiko yanayoitwa **manung'ung'uniko**. Unaweza kuiwasilisha wakati wowote kwa kuwapiga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**.

Je, itakuaje kama hufurahishwi na jinsi malalamiko yako yanavyoshughulikiwa? Unaweza kuomba **Mapitio ya Malalamiko**. Mtu ambaye hakushughulikia malalamiko yako atapitia kesi yako. Atachunguza ili kuona kama ilishughulikiwa kwa haki. Utapata barua inayosema walichoamua.

# Je, Unahitaji Msaada?

### Huduma kwa Wateja ya Vermont Health Connect na Green Mountain Care

Huduma kwa Wateja wa Vermont Health Connect na Green Mountain Care wapo kukusaidia. Wanaweza kujibu maswali kuhusu mpango wako. Wanaweza kukusaidia kuchagua au kumbadilisha daktari/PCP wako. Wanaweza kukusaidia ikiwa una matatizo ya kupata huduma za afya.

Huduma kwa Wateja huanza kazi saa 2:00 asubuhi (8:00 am) hadi saa 10:30 jioni (4:30pm), Jumatatu hadi Ijumaa. Hatufanyi kazi siku za sikukuu. Piga simu **1-800-250-8427** au TDD 1-888-834-7898.

**Ripoti mabadiliko ndani ya siku 10 baada ya mabadiliko kutokea:**

- Mabadiliko ya mapato yako au kaya;
- Mabadiliko ya anwani;
- Kuzaliwa au kuwaasili watoto;
- Vifo; na
- Bima nyingine ya afya utakayopata.

## Ofisi ya Utetezi wa Huduma za Afya (HCA)

Ofisi ya Utetezi wa Huduma za Afya husaidia katika matatizo ya huduma za afya. Wanaweza pia kukusaidia katika malalamiko, rufaa, na usikilizaji wa shauri la haki. Piga simu **1-800-917-7787**.

## Taarifa za Ziada

Tunafurahi kutoa taarifa kuhusu mipango yetu, huduma na watoa huduma. Soma kitabu hiki cha mwongozo. Au piga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427. AU** tembelea tovuti ya DVHA.

## Mipango Mingine

Kuna mipango na huduma nyinginezo kwa watoto, watu wazima na familia. Baadhi ya mipango itakupa usafiri kwenda kwenye huduma zake. Pata maelezo zaidi kwa kupiga simu Huduma kwa Wateja kwa **1-800-250-8427**. Lazima utimize kanuni nyingi zaidi ili kupata baadhi ya mipango. Je, una maswali au ungependa kujua ikiwa unatimiza kanuni hizo? Piga simu kwenye mpango unaotaka. Majina na namba zao ziko hapa chini.

### Huduma za Mchana kwa Watu Wazima

Huduma za Mchana kwa Watu Wazima huwasaidia watu wazima na watu wazima wenye ulemavu kukaa katika nyumba zao wenyewe. Huduma za Mchana kwa Watu Wazima hufanyika katika vituo vya mchana. Ni mahali salama ambapo watu wanaweza kupata huduma za afya na kijamii. Piga simu kwenye Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-2401. AU** nenda kwenye tovuti ya huduma za mchana kwa watu wazima.

### Mpango wa Huduma za Wahudumu

Mpango huu huwasaidia watu wazima wenye ulemavu wanaohitaji msaada wa kimaumbile katika shughuli za kila siku. Unawaajiri, unawafunza, unawasimamia na kupanga wahudumu wako binafsi. Piga simu kwenye Idara ya Watu wenye Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-2401. AU** nenda kwenye tovuti ya mpango wa huduma za mhudumu.

### Huduma Jumuishi za Watoto (CIS)

Hii husaidia wanawake ambao ni wajawazito au wale ambao wamepata mtoto. Pia, huzisaidia familia zenye watoto kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka sita. Wanasaidia kwa:

- kazi ya kijamii na msaada wa familia,
- afya ya mama/mtoto na uuguzi,
- ukuaji wa mtoto na kuwasaidia watoto kuanzia kuzaliwa hadi miaka 3 waliodumaa,
- afya ya akili ya utotoni na familia,
- huduma za watoto, na
- mambo mengine kama vile kula vizuri, matatizo ya kuzungumza na ya lugha.

Piga simu kwenye Idara ya Maendeleo ya Watoto na Familia kwa **802-241-3110** au **1-800-649-2642. AU** nenda kwenye **tovuti ya huduma jumuishi za watoto.**

### Huduma Jumuishi za Watoto - Afua ya Mapema (CIS-EI)

Mpango huu ni kwa watoto wenye umri wa miaka 3 ambao wana ulemavu. **AU** kwa watoto walio nyuma ya watoto wengine wa umri wao. Huwasaidia watoto wadogo, watoto wachanga, na familia. Piga simu kwenye Mtandao wa Familia wa Vermont kwa **1-800-800-4005**.

### Huduma za Matunzo Binafsi ya Watoto

Huduma Binafsi ya Watoto ni huduma ya Medicaid kwa watu wenye umri chini ya miaka 21. Lazima wawe na ulemavu mkubwa wa muda mrefu au tatizo la kiafya. Ni lazima wahakikishe anafanya mambo ambayo watu wa umri wao wanapaswa kufanya. Ni lazima wahakikishe anafanya shughuli za maisha ya kila siku, kama kula, kuvaa, kwenda bafuni pekeyake. Mpango huo husaidia kwa kutoa huduma binafsi ya mtoto. Piga simu **1-800-660-4427** au **802-863-7338. AU** nenda kwenye tovuti ya huduma za watoto binafsi.

### Watoto wenye Mahitaji Maalum ya Afya (CSHN)

CSHN husaidia kupanga uangalizi wa watoto wenye mahitaji maalum ya kiafya. Inaweza kusaidia kwenye mipango na huduma hizi:
Uratibu wa huduma
Huduma za Matunzo Binafsi ya Watoto
Huduma za Lishe kwa Jamii
Mpango wa Uchunguzi wa watoto Wachanga
Mpango wa Uuguzi wa Watoto wa Hi-Tech
Mpango wa Huduma ya Matunzo kwa Watoto
Utambuzi na Afua ya Mapema wa Kusikia wa Vermont
Piga simu **1-800-660-4427** au **802-863-7338**, AU nenda kwenye tovuti ya watoto wenye mahitaji maalum ya kiafya.

### Machaguo ya Uangalizi

Huu ni mpango wa huduma ya muda mrefu. Inalipia matunzo na msaada kwa watu wazima wa Vermont na watu wenye ulemavu wa kimaumbile. Mpango huwasaidia watu katika shughuli za kila siku. Wanaweza kuwa wanaishi nyumbani, katika matunzo yaliyoimarishwa kwenye makazi, au katika makao ya wazee. Watoa huduma ni:

- Vituo vya Mchana kwa Watu Wazima
- Mashirika ya Eneo kuhusu Wazee
- Nyumba za Kuishi Zinazosaidiwa
- Mashirika ya Afya ya Nyumbani
- Vituo vya Uuguzi
- Nyumba za Huduma za Makazi

Piga simu **802-241-0294**. **AU** nenda kwenye tovuti ya chaguo za matunzo.

### Huduma za Ulemavu wa Ukuaji

Huwasaidia watu wa umri wowote wenye ulemavu wa ukuaji. Huwasaidia kuishi nyumbani na familia zao. Huduma zinajumuisha usimamizi wa tatizo, huduma za ajira,

misaada ya jamii, na mapumziko. Kupumzika hutoa huduma wakati familia zinachukua mapumziko mafupi. Piga simu kwenye Idara ya Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-0304. AU** nenda kwenye tovuti ya huduma za walemavu wa ukuaji.

### Mpango wa Msaada wa Kifedha

Huzisaidia familia kulipa gharama za huduma ya afya ya mtoto wao ambayo bima hailipii. Huduma lazima ziwe zimeagizwa au zimeidhinishwa na kliniki ya Mahitaji Maalum ya Afya ya Watoto. Piga simu kwenye Idara ya Afya ya Vermont kwa **1-800-660-4427** au **802-863-7338**. **AU** nenda kwenye tovuti hii kwa taarifa zaidi.

### Ufadhili Rahisi wa Familia

Hii ni kwa watu wa umri wowote wenye ulemavu wa ukuaji ambao wanaishi na familia. **AU** kwa familia ambazo zinaishi na kumsaidia mwanafamilia mwenye ulemavu wa ukuaji. Familia huamua ni huduma gani ambazo fedha zitalipia. Piga simu kwa Idara ya Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea, Idara ya Huduma za Ukuaji kwa **802-241-0304. AU** nenda kwenye tovuti ya ufadhili wa familia inayoweza kubadilika.

### Huduma za Uuguzi za Teknolojia ya Hali ya Juu

Huu ni mpango mkubwa wa uuguzi wa nyumbani. Ni kwa watu wanaohitaji teknolojia ili kuishi au wana mahitaji magumu ya kimatibabu. Mpango huwasaidia watu kutoka hospitali au taasisi kuishi nyumbani kwao. Kwa watu **wenye umri wa zaidi ya miaka 21**, pigia simu Idara ya Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-0294. AU** nenda kwenye tovuti ya huduma za teknolojia ya juu kwa watu wazima.
Kwa watu **wenye umri chini ya miaka 21**, wapigie simu Mpango wa Utunzaji wa Nyumbani wa Teknolojia ya Juu kwa Watoto. Piga simu **1-800-660-4427** au **802-863-7338. AU** nenda kwenye tovuti ya uuguzi wa teknolojia ya juu kwa watoto.

### Huduma za Wahudumu wa Nyumbani

Hii huwasaidia watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi wenye ulemavu. Mpango huo husaidia kwa mahitaji binafsi au kazi za nyumbani ili watu waweze kuishi nyumbani. Huduma hujumuisha ununuzi, usafi, na kufua. Wapigie simu Idara ya Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-0294. AU** nenda kwenye tovuti ya huduma za wahudumu wa nyumbani.

### Mipango ya Hub na Spoke

Mfumo wa Hub na Spoke wa Uangalizi wa ugonjwa wa matumizi ya opioidi (OUD) umeundwa kutengeneza mfumo jumuishi kati ya mazingira mawili ambapo Dawa za Ugonjwa wa Matumizi ya Opioidi (MOUD) hutolewa na kuratibu mipangilio ya mifumo ya matibabu ya MOUD na huduma pana za afya na binadamu. Mazingira mawili ya MOUD ni: "Mipango ya Matibabu ya Opioidi (OTPs)" inayojulikana katika Vermont kama vile Hub, ambapo dawa hutolewa na wagonjwa wanaweza kuonekana kila siku wakati uhusiano zaidi umeonyeshwa; na Spoke ni "Matibabu ya Opioidi ya Ofisini (OBOT)" ambapo dawa huagizwa na wagonjwa huonwa mara chache. Huduma zinajumuisha dawa, uchunguzi wa vichocheo vya kijamii vya afya, kama vile nyumba na upatikanaji wa chakula. Katika Hub na Spokes, washauri, wasimamizi wa kesi na wauguzi walitoa ushauri nasaha na uangalizi wa timu ili kuratibu na kutoa huduma ya afya ya mtu mzima. Kiwango cha wastani hadi

kidogo cha ugumu wa uraibu kinaweza kutibiwa katika Spoke ambazo ni ofisi za madaktari wa asili au kliniki maalum za uraibu. Ili kuwasiliana na MOUD watu wa kuwasiliana nao wanaweza kupatikana kwa kutembelea ukurasa wa mawasiliano ya mpango makini. Kwa taarifa za kawaida, Kituo cha Msaada cha Vermont na cha Msaada wa Pombe na Dawa za Kulevya kinaweza kupatikana kwa kutembelea tovuti hii.

### Mpango wa Vermont wa Kugundua na Afua ya Mapema wa Kusikia

Hii inatoa msaada, mafunzo na msaada wa matunzo kwa familia na watoto wao wachanga, na watoa huduma wa jamii. Wanasaidia kutafuta huduma za upimaji na afua ya mapema. Piga simu **1-800-537-0076** au **802-651-1872. AU** nenda kwenye tovuti ya mpango wa Vermont wa ugunduzi na afua ya mapema wa kusikia.

### Afya ya Akili

Jimbo la Vermont hufanya kazi na mashirika katika jimbo zima. Mashirika hayo yanatoa huduma za afya ya akili kuwasaidia watu na familia zao. Hii inaweza kuwa tatizo kubwa la hisia, ugonjwa wa akili, au shida kubwa za tabia. Wanaweza pia kusaidia kupata huduma ya ukuaji, vitanda vya dharura, na huduma za hospitali. Piga simu kwenye Idara ya Afya ya Akili kwa **802-241-0090. AU** nenda kwenye tovuti ya afya ya akili. Huduma zinajumuisha:

- Huduma za Wagonjwa wa Nje Watu Wazima - Huduma zinaweza kujumuisha tathmini, ushauri nasaha, kuandikiwa dawa na ufuatiliaji. Inaweza kujumuisha huduma kwa watu wenye umri wa miaka 60 au zaidi wenye mahitaji ya afya ya akili. Unaweza kuwekwa kwenye orodha ya wanaosubiri.

- Huduma za Watoto, Vijana na Familia - Hizi ni huduma na misaada kwa familia ambazo watoto au vijana wana matatizo ya afya ya akili. Wanawasaidia kuishi, kujifunza, na kukua wakiwa na afya njema shuleni mwao na katika jamii. Huduma zinajumuisha uchunguzi, kinga, misaada ya kijamii, matibabu, ushauri na majibu ya dharura.

- Urekebishaji na Matibabu ya Jamii - Mpango huu huwasaidia watu kuishi katika jamii zao kwa familia, marafiki na majirani. Huduma ni kwa watu wazima pekee wenye aina fulani za ugonjwa mkali wa akili. Lazima pia watimize kanuni zingine.

- Huduma za Dharura **- Hizi** ni **huduma za dharura za afya ya akili**. Ziko wazi saa 24 **kwa siku, siku** 7 **kwa wiki**. Hu**duma zinaweza kujumuisha msaada kwa njia ya simu,** ukaguzi**wa ana kwa ana, rufaa, na mashauriano.**

## Mpango wa Majeraha ya Kiwewe cha Ubongo

Mpango huu huwasaidia watu wenye umri wa miaka 16 au zaidi wenye jeraha la wastani hadi kubwa la ubongo. Unasaidia watu kurudi nyumbani kutoka hospitali na katika vituo. Huwasaidia watu kujitegemea kadri iwezekanavyo na kurudi kazini. Wapigie simu Idara ya Ulemavu, Wazee na Maisha ya Kujitegemea kwa **802-241-0294. AU** nenda kwenye tovuti ya mpango wa majeraha ya ubongo.

### Mpango wa Wanawake, Watoto wachanga na Watoto (WIC)

Huu ni mpango wa lishe kwa watoto wachanga na watoto hadi umri wa miaka 5. Pia, ni kwa ajili ya watu ambao ni wajawazito au wale ambao wamepata mtoto hivi karibuni. Hutoa chakula cha afya na hufundisha kuhusu ulaji bora na kunyonyesha. Mtu yeyote katika Medicaid anaweza kupata programu ya WIC. Nenda kwenye tovuti ya wic. **AU** tuma neno VTWIC kwenda **855-11**.

**Pata maelezo zaidi kuhusu msaada katika jamii yako kwenye tovuti ya 211.**